



CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM  
CHUO KISHIRIKI CHA ELIMU MKWAWA

# Matukio ya wiki

25 APRILI - 1 MEI 2022

Yaliyomo

## 01 SEMINA

Elimu maalum na ujumuishaji

## 02 MACHAPISHO

Wanataaluma watatu wametoa machapisho

## 03 MEI MOSI

MUCE yashiriki siku ya wafanyakazi duniani, 2022

Imeandaliwa na Kitengo cha Habari na Masoko, MUCE

Hekima ni Uhuru  
[www.muce.ac.tz](http://www.muce.ac.tz)

# Semina ya elimu maalum na ujumuishaji



Rasi wa Chuo, Prof. Esther W. Dungumaro, alikutana na wafanyakazi waendeshaji wa Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa tarehe 30 Aprili 2022 kuzungumia masuala yanayohusu changamoto za wanafunzi wenye mahitaji maalum. Semina hiyo ni matokeo ya mkutano wa Rasi wa Chuo na wanafunzi wenye mahitaji maalum uliofanyika tarehe 9 Aprili 2022. Rasi wa Chuo baada ya kufungua semina hiyo, aliwasilisha mada yake kuhusu sera na miongozo ya nchi kwa watu wenye mahitaji maalum. Katika uwasilishaji wake alizungumzia Sera ya Taifa Ya Maendeleo Na Huduma Kwa Watu Wenye Ulemavu (2004) na Mkakati wa Taifa wa Miaka Mitano wa Elimu Jumuishi 2021/22-2025/26.

Mada zingine zilizowasilishwa katika semina hiyo ni istilahi zinazotumika katika taaluma ya elimu maalum na historia fupi ya elimu maalum, zilizowasilishwa na Dkt. Orestes Kapinga; namna ya kuwatambua watu wenye mahitaji maalum, kuwasiliana nao na kutatua changamoto zao, zilizowasilishwa na Dkt. Vicent Jalang'o; na miongozo kuhusu watu wenye mahitaji maalum mahali pa kazi iliyowasilishwa na Bw. Edwin Lyagoda.

# Machapisho



Wanataaluma wawili: Dkt. Selina Mkimbili na Bw. John Mlyahilu wamefanikiwa kutoa machapisho yao kwenye majarida mbalimbali ya Kimataifa.

Chuo kinawapongeza sana.

Mkimbili, Selina. (2022). *Do biology syllabi provide opportunities for secondary school students to engage with critical thinking skills?* *Journal of Biological Education*. DOI: 10.1080/00219266.2022.2067582.

Mlyahilu, John, Mlyahilu, Joseph, Lee, Jae Euth and Kim, Young Bong. (2022). Morphological geodesic active contour algorithm for the segmentation of the histogram-equalized welding bead image edges. DOI: 10.1049/ipr2.12517.



# MEI MOJI, 2022



Happy International  
**Workers' Day**

*Where there is no labour,  
there are no fruits of hard work to enjoy.*

Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilishiriki Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani tarehe 1 Mei 2022, ambapo kwa mkoa wa Iringa, maadhimisho hayo yalifanyika Ifunda. Katika maadhimisho hayo, Bw. Tom Pascal Mhongole alitangazwa kuwa mfanyakazi bora wa Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa kwa mwaka 2022. Chuo kinampongeza sana Bw. Tom Pascal Mhongole kwa utendaji wake uliopelekea kuwa mfanyakazi bora.



## **Bw. Tom Pascal Mhongole Mfanyakazi Bora MUCE 2022**

Bw. Tom Pascal Mhongole ni mfanyakazi mwendeshaji kwenye Kitengo cha Mipango na Maendeleo. Amejiriwa kama Afisa Mipango wa Chuo.